



UTAFITI WA KIMATAIFA SHULENI KUHUSU AFYA YA WANAFUNZI

[GLOBAL SCHOOL-BASED STUDENT HEALTH SURVEY]

TANZANIA, 2006

UTAFITI WA KIMATAIFA SHULENI KUHUSU AFYA YA WANAFUNZI

Utafiti huu unahus afya yako na tabia zinazoweza kuathiri afya yako. Wanafunzi wengi nchini wanashiriki katika utafiti huu. Wanafunzi katika nchi nyingine nyingi duniani pia wanashiriki katika utafiti huu. Taarifa utakayotoa itatumika kwa kuandaa mikakati mizuri ya afya kwa watoto na vijana kama wewe.

USIANDIKE jina lako kwenye karatasi hii ya maswali au karatasi ya majawabu. Majawabu yote utakayotoa yatahifadhiwa kwa siri. Hakuna atakayefahamu jinsi unavyojibu. Jibu maswali kuzingatia mambo halisi unayoyafahamu au unayoyafanya. Hakuna majawabu sahihi au makosa.

Kujaza fomu hii ni hiari. Matokeo au maksi zako za darasani hazitaathirika kwa kujibu au kutojibu maswali haya. Hakikisha kuwa unajibu maswali yote.

Hakikisha unasoma kila swali. Jaza miduara iliyopo kwenye karatasi ya majibu inayoendana na jawabu lako. Tumia penseli uliyopewa tu. Ukimaliza, fuata maelekezo ya mtu anayekupatia fomu hii ya maswali.









Hapa ni mfano wa jinsi ya kujaza miduara hiyo:

Jaza miduara kwa kuweka kivuli kama hivi  Siyo kama  au  au 

Swali

1. Je, samaki wanaishi katika maji?
 - A. Ndiyo
 - B. Hapana

Jawabu

1.        

ASANTE SANA KWA KUSHIRIKI KWAKO

1. Je, una umri gani?
 - A. Miaka 11 au pungufu
 - B. Miaka 12
 - C. Miaka 13
 - D. Miaka 14
 - E. Miaka 15
 - F. Miaka 16 au zaidi
2. Jinsia yako ni ipi?
 - A. Mvulana
 - B. Msichana
3. Unasoma darasa la ngapi?
 - A. Darasa la V
 - B. Darasa la VI
 - C. Darasa la VII
 - D. Darasa jingine

Maswali 2 yafuatayo yanahusu urefu na uzito wako.

4. Wewe una urefu gani usipovaa viatu vyako?

KWENYE KARATASI YA MAJAWABU, ANDIKA UREFU WAKO SEHEMU YA JUU YA KILA SAFU. HALAFU JAZA MDUARA CHINI YA KILA NAMBA.

Mfano

Urefu (sm)		
1	5	3
<input type="radio"/>	<input type="radio"/>	<input type="radio"/>
<input checked="" type="radio"/>	<input type="radio"/>	<input type="radio"/>
<input type="radio"/>	<input type="radio"/>	<input type="radio"/>
	<input type="radio"/>	<input checked="" type="radio"/>
	<input type="radio"/>	<input type="radio"/>
	<input checked="" type="radio"/>	<input type="radio"/>
	<input type="radio"/>	<input type="radio"/>
	<input type="radio"/>	<input type="radio"/>
	<input type="radio"/>	<input type="radio"/>
	<input type="radio"/>	<input type="radio"/>
<input type="radio"/>	Sijui	

5. Wewe una uzito kiasi gani usipovaa viatu vyako?

KWENYE KARATASI YA MAJAWABU, ANDIKA UREFU WAKO SEHEMU YA JUU YA KILA SAFU. HALAFU JAZA MDUARA CHINI YA KILA NAMBA.

Mfano

Uzito (kg)		
0	5	2
<input checked="" type="radio"/>	<input type="radio"/>	<input type="radio"/>
<input type="radio"/>	<input type="radio"/>	<input type="radio"/>
<input type="radio"/>	<input type="radio"/>	<input checked="" type="radio"/>
	<input type="radio"/>	<input type="radio"/>
	<input type="radio"/>	<input type="radio"/>
	<input checked="" type="radio"/>	<input type="radio"/>
	<input type="radio"/>	<input type="radio"/>
	<input type="radio"/>	<input type="radio"/>
	<input type="radio"/>	<input type="radio"/>
	<input type="radio"/>	<input type="radio"/>
<input type="radio"/>	Sijui	

Maswali 3 yafuatayo yanahusu kukaa na njaa na milo uliyokula.

6. Katika siku 30 zilizopita, mara ngapi ulishinda na njaa kutokana na ukosefu wa chakula nyumbani?

- A. Sikuwahi
- B. Mara chache sana
- C. Mara chache
- D. Mara nyingi
- E. Mara nyingi sana

7. Katika siku 30 zilizopita, mara ngapi ulipata kifungua kinywa asubuhi?

- A. Sikuwahi
- B. Mara chache sana
- C. Mara chache
- D. Mara nyingi
- E. Mara nyingi sana

8. Katika siku 30 zilizopita, mara ngapi ulikula chakula cha mchana shuleni?

- A. Sikuwahi
- B. Mara chache sana
- C. Mara chache
- D. Mara nyingi
- E. Mara nyingi sana

Maswali 2 yafuatayo yanahusu aina ya vyakula ulivyokula.

9. Katika siku 30 zilizopita, mara ngapi kwa siku **kwa kawaida** ulikula matunda, kama vile ndizi mbivu, machungwa, mapapai, maembe, au mananasi?

- A. Sikula matunda katika siku 30 zilizopita
- B. Pungufu ya mara 1 kwa siku
- C. Mara 1 kwa siku
- D. Mara 2 kwa siku
- E. Mara 3 kwa siku
- F. Mara 4 kwa siku
- G. Mara 5 au zaidi kwa siku

10. Katika siku 30 zilizopita, mara ngapi kwa siku **kwa kawaida** ulikula mboga za majani kama vile mchicha, kisamvu, majani ya maboga, kabichi spinach, bamia, au karoti?

- A. Sikula mboga za majani katika siku 30 zilizopita
- B. Pungufu ya mara 1 kwa siku
- C. Mara 1 kwa siku
- D. Mara 2 kwa siku
- E. Mara 3 kwa siku
- F. Mara 4 kwa siku
- G. Mara 5 au zaidi kwa siku

Maswali yafuatayo yanahusu nini ulichojifunza shuleni.

11. Katika mwaka huu wa shule, ulifundishwa katika somo lolote faida za lishe bora?
- A. Ndiyo
 - B. Hapana
 - C. Sijui

Maswali 7 yafuatayo yanahusu tabia za usafi wa mwili.

12. Katika siku 30 zilizopita, mara ngapi kwa siku **kawaida** ulisafisha au kupiga mswaki meno yako?
- A. Sikusafisha au kupiga mswaki meno yangu katika siku 30 zilizopita
 - B. Mara 1 kwa siku
 - C. Mara 2 kwa siku
 - D. Mara 3 kwa siku
 - E. Mara 4 au zaidi kwa siku
13. Katika siku 30 zilizopita, mara ngapi ulinawa mikono yako kabla ya kula?
- A. Sikuwahi
 - B. Mara chache sana
 - C. Mara chache
 - D. Mara nyingi
 - E. Kila wakati
14. Katika siku 30 zilizopita, mara ngapi ulinawa mikono yako baada ya kutumia choo?
- A. Sikuwahi
 - B. Mara chache sana
 - C. Mara chache
 - D. Mara nyingi
 - E. Kila wakati

15. Katika siku 30 zilizopita, mara ngapi ulitumia sabuni uliponawa mikono yako?

- A. Sikuwahi
- B. Mara chache sana
- C. Mara chache
- D. Mara nyingi
- E. Kila mara

16. Je, ni rahisi kupata vyoo unapohitaji kutumia ukiwa shuleni?

- A. Hakuna vyoo shuleni
- B. Ndiyo
- C. Hapana

17. Kuna chanzo cha maji safi ya kunywa shuleni?

- A. Ndiyo
- B. Hapana

18. Katika mwaka huu wa masomo, ulifundishwa katika somo lolote umuhimu wa kunawa mikono?

- A. Ndiyo
- B. Hapana
- C. Sijui

Maswali 2 yafuatayo yanahusu minyoo

19. Katika mwaka huu wa masomo, ulifundishwa katika somo lolote jinsi ya kuepuka minyoo?

- A. Ndiyo
- B. Hapana
- C. Sijui

20. Katika mwaka huu wa masomo, ulifundishwa katika somo lolote mahali pa kupata tiba ya minyoo?

- A. Ndiyo
- B. Hapana
- C. Sijui

Swali lifuatalo linahusu kushambuliwa mwilini. Shambulio mwilini hutokea wakati mtu mmoja au zaidi anapomgonga au kumpiga mtu mwingine, au kama mtu mmoja au zaidi anamuumiza mtu mwingine kwa kutumia silaha (kama fimbo, kisu, au bunduki). Siyo shambulio wakati wanafunzi wawili wanaokaribiana nguvu wanapoamua kupigana.

21. Katika miezi 12 iliyopita, mara ngapi ulishambuliwa mwilini?

- A. Mara 0
- B. Mara 1
- C. Mara 2 au 3
- D. Mara 4 au 5
- E. Mara 6 au 7
- F. Mara 8 au 9
- G. Mara 10 au 11
- H. Mara 12 au zaidi

Swali lifuatalo linahusu kupigana. Kupigana hutokea wakati wanafunzi wawili au zaidi wanaokaribiana nguvu wanapoamua kupigana.

22. Katika miezi 12 iliyopita, mara ngapi ulishiriki katika kupigana?

- A. Mara 0
- B. Mara 1
- C. Mara 2 au 3
- D. Mara 4 au 5
- E. Mara 6 au 7
- F. Mara 8 au 9
- G. Mara 10 au 11
- H. Mara 12 au zaidi

Maswali 5 yafuatayo yanahusu jeraha baya zaidi ulilopata katika miezi 12 iliyopita. Jeraha ni baya kama linakufanya ukose angalau siku moja nzima ya shughuli za kawaida (kama vile shule, michezo, au kazi) au linapohitaji kutibiwa na daktari au muuguzi.

23. Katika miezi 12 iliyopita, mara ngapi ulijeruhiwa vibaya?

- A. Mara 0
- B. Mara 1
- C. Mara 2 au 3
- D. Mara 4 au 5
- E. Mara 6 au 7
- F. Mara 8 au 9
- G. Mara 10 au 11
- H. Mara 12 au zaidi

24. Katika miezi 12 iliyopita, **ulikuwa unafanya nini** wakati jeraha hilo baya lilipokupata?

- A. Sikujeruhiwa vibaya katika miezi 12 iliyopita
- B. Kucheza au kujifunza mchezo
- C. Kutembea au kukimbia, lakini siyo kucheza au kujifunza mchezo
- D. Kuendesha baiskeli, pikipiki, mtumbwi, mkokoteni, toroli, au punda
- E. Kupakia au kuendesha gari au motokaa aina nyingine
- F. Kufanya kazi yoyote ya kulipwa au ya kutolipwa, ikiwemo kazi za ndani, kazi za nje, au kupika
- G. Hakuna
- H. Kitu kingine

25. Katika miezi 12 iliyopita, **nini kilikuwa chanzo kikuu cha** jeraha baya kabisa lililokupata?

- A. Sikupata jeraha baya katika miezi 12 iliyopita
- B. Nilihusika katika ajali ya motokaa au kugongwa na motokaa
- C. Nilianguka
- D. Kitu fulani kiliniangukia au kunigonga
- E. Nilikuwa napigana na mtu
- F. Nilivamiwa, kushambuliwa au kuteswa na mtu
- G. Niliungua moto au kuukaribia moto au kitu cha moto
- H. Ni kitu kingine kilichosababisha jeraha langu

26. Katika miezi 12 iliyopita, **ni vipi** hilo jeraha baya kabisa lilivyokupata?

- A. Sikupata jeraha baya katika miezi 12 iliyopita
- B. Niliumia mwenyewe kwa bahati mbaya
- C. Mtu mwingine aliniumiza kwa bahati mbaya
- D. Nilijiumiza mwenyewe kwa makusudi
- E. Mtu mwingine aliniumiza kwa makusudi

27. Katika miezi 12 iliyopita, ni jeraha **lipi** baya kabisa lililokupata?

- A. Sikupata jeraha baya katika miezi 12 iliyopita
- B. Nilivunjika mfupa au kuteguka kiungo cha mifupa
- C. Nilikatwa, kutobolewa, au kuchomwa kitu
- D. Nilipata uvimbe au jeraha jingine la kichwa au shingo, nilizimia, au sikuweza kupumua
- E. Nilipata jeraha la kupigwa risasi
- F. Niliungua vibaya
- G. Nilipoteza sehemu ya unyayo, mguu, kiganja, au mkono mzima
- H. Nilipatwa na kitu kingine

Maswali 2 yafuatayo yanahusu kunyanyaswa. Kunyanyaswa hutokea wakati mwanafunzi mmoja au kikundi cha wanafunzi wanasema au kufanya mambo yasiyopendeza kwa mwanafunzi mwingine. Ni kunyanyaswa pia wakati mwanafunzi anataniwa sana kwa hali isiyopendeza au mwanafunzi anapotengwa kwenye vitu kwa makusudi. Siyo kunyanyaswa wakati wanafunzi wawili wanaokaribiana nguvu wanapobishana au kupigana au kutaniana kirafiki na kimzaha.

28. Katika siku 30 zilizopita, kwa siku ngapi ulinyanyaswa?

- A. Siku 0
- B. Siku 1 au 2
- C. Siku 3 hadi 5
- D. Siku 6 hadi 9
- E. Siku 10 hadi 19
- F. Siku 20 hadi 29
- G. Siku zote 30

29. Katika siku hizo 30 zilizopita, ulinyanyaswa vipi **mara nyingi**?

- A. Sikunyanyaswa katika siku hizo 30
- B. Nilipigwa, kusukumwa, kupigwa kikumbo, au kufungiwa ndani
- C. Nilichekwa kutokana na kabila au rangi yangu
- D. Nilichekwa kutokana na dini yangu
- E. Nilichekwa kwa kutaniwa, kupigwa vijembe au kupigwa kuhusu maswala ya mapenzi
- F. Nilitengwa kwenye vitu kwa makusudi au kupuuzwa kabisa
- G. Nilichekwa kutokana na umbile langu au sura yangu
- H. Nilinyanyaswa kwa njia nyingine

Swali lifuatalo linahusu mambo ya kiusalama.

30. Katika mwaka huu wa masomo, ulifundishwa katika somo lolote mbinu za huduma ya kwanza endapo wewe mwenyewe au mtu mwingine anaumia?

- A. Ndiyo
- B. Hapana
- C. Sijui

Maswali 6 yafuatayo yanahusu hisia zako na mahusiano yako ya kirafiki.

31. Katika miezi 12 iliyopita, mara ngapi ulijisikia mpweke?

- A. Hakuna
- B. Mara chache sana
- C. Mara chache
- D. Muda mwingi
- E. Daima

32. Katika miezi 12 iliyopita, mara ngapi ulipatwa na wasiwasi sana juu ya jambo fulani kiasi cha kukosa usingizi usiku?

- A. Hakuna
- B. Mara chache sana
- C. Mara chache
- D. Muda mwingi
- E. Daima

33. Katika miezi 12 iliyopita, uliwahi kusunoneka sana au kukata tamaa karibia kila siku kwa **wiki mbili au zaidi mfululizo** kiasi cha kuacha kufanya shughuli zako za kawaida?

- A. Ndiyo
- B. Hapana

34. Katika miezi 12 iliyopita, uliwahi kutamani **kiuhakika** kujiua?

- A. Ndiyo
- B. Hapana

35. Katika miezi 12 iliyopita, uliandaa mpango wa jinsi ya kujiua?

- A. Ndiyo
- B. Hapana

36. Unao marafiki wa karibu wangapi?

- A. 0
- B. 1
- C. 2
- D. 3 au zaidi

Maswali 14 yafuatayo yanahusu matumizi ya sigara na tumbaku nyingine.

37. Ulikuwa na umri gani ulipojaribu mara ya kwanza kuvuta sigara?

- A. Sijawahi kuvuta sigara
- B. Miaka 7 au pungufu
- C. Miaka 8 au 9
- D. Miaka 10 au 11
- E. Miaka 12 au 13
- F. Miaka 14 au 15
- G. Miaka 16 au zaidi

38. Katika siku 30 zilizopita, kwa siku ngapi ulivuta sigara?

- A. Siku 0
- B. Siku 1 au 2
- C. Siku 3 hadi 5
- D. Siku 6 hadi 9
- E. Siku 10 hadi 19
- F. Siku 20 hadi 29
- G. Siku zote 30

39. Katika siku 30 zilizopita, kwa siku ngapi ulitumia aina nyingine yoyote ya tumbaku, kama vile msokoto, ugoro au tumbaku ya kutafuna?

- A. Siku 0
- B. Siku 1 au 2
- C. Siku 3 hadi 5
- D. Siku 6 hadi 9
- E. Siku 10 hadi 19
- F. Siku 20 hadi 29
- G. Siku zote 30

40. Katika siku hizo 30 zilizopita, ulizipataje **kwa kawaida** sigara zako? CHAGUA JAWABU MOJA TU.

- A. Sikuvuta sigara katika hizo siku 30 zilizopita
- B. Nilizinunua katika kibanda, duka, au kutoka kwa muuzaji wa barabarani
- C. Nilizinunua kwenye mashine ya kuuzia
- D. Nilimpa mtu mwingine fedha kuninunulia
- E. Niliziazima kutoka kwa mtu mwingine
- F. Niliziiba
- G. Nilipewa na mtu mzima
- H. Nilizipata kwa njia nyingine

41. Ni wapi kwa **kawaida** unapovutia sigara? CHAGUA JAWABU MOJA TU.

- A. Sijawahi kuvuta sigara
- B. Nyumbani
- C. Shuleni
- D. Kazini
- E. Nyumbani kwa marafiki
- F. Kwenye mikusanyiko ya jamii
- G. Kwenye sehemu za umma, kama vile bustani za mapumziko, madukani, na vijiwe vya mtaani
- H. Sehemu nyingine

42. Katika miezi 12 iliyopita, uliwahi kujaribu kuacha kuvuta sigara?

- A. Sijawahi kuvuta sigara
- B. Sikuvuta sigara katika miezi 12 iliyopita
- C. Ndiyo
- D. Hapana

43. Unafikiri kuwa kuvuta sigara kunaweza kuathiri afya yako?

- A. Hapana kabisa
- B. Pengine hapana
- C. Pengine ndiyo
- D. Hakika ndiyo

44. Unafikiri kuwa moshi wa sigara kutoka kwa watu wengine unaweza kuathiri afya yako?

- A. Hapana kabisa
- B. Pengine hapana
- C. Pengine ndiyo
- D. Hakika ndiyo

45. Mtu akishaanza kuvuta sigara, unadhani ni vigumu kuacha kabisa?

- A. Hapana kabisa
- B. Pengine hapana
- C. Pengine ndiyo
- D. Hakika ndiyo

46. Katika siku 7 zilizopita, kwa siku ngapi watu wamevuta sigara mahali ulipo?

- A. Siku 0
- B. Siku 1 au 2
- C. Siku 3 au 4
- D. Siku 5 hadi 6
- E. Siku zote 7

47. Nani kati ya wazazi au walezi wako wanatumia aina yoyote ya tumbaku?

- A. Hakuna
- B. Baba au mlezi wa kiume
- C. Mama au mlezi wa kike
- D. Wote
- E. Sijui

48. Kuna rafiki yako wa karibu yeyote anayevuta sigara?

- A. Hakuna kati yao
- B. Wachache kati yao
- C. Wengi kati yao
- D. Wote

49. Kuna yeyote katika familia yako aliyejadiliana nawe kuhusu madhara ya kuvuta sigara?

- A. Ndiyo
- B. Hapana

50. Katika mwaka huu wa shule, ulifundishwa katika somo lolote kuhusu hatari za kuvuta sigara?

- A. Ndiyo
- B. Hapana
- C. Sijui

Maswali 11 yafuatayo yanahusu kunywa pombe. Hii inahusu kunywa pombe kama mbege, kimpumu, mnazi, dengerua, au ulanzi. Kunywa pombe haihusu kuonja mvinyo kidogo kwa malengo ya kidini.

51. Ulikuwa na umri gani ulipojaribu kwa mara ya kwanza kunywa pombe zaidi ya kuonja kidogo?

- A. Sijawahi kunywa pombe zaidi ya kuonja kidogo
- B. Miaka 7 au pungufu
- C. Miaka 8 au 9
- D. Miaka 10 au 11
- E. Miaka 12 au 13
- F. Miaka 14 au 15
- G. Miaka 16 au zaidi

52. Katika siku 30 zilizopita, kwa siku ngapi ulipata kinywaji chenye pombe angalau mara moja?

- A. Siku 0
- B. Siku 1 au 2
- C. Siku 3 hadi 5
- D. Siku 6 hadi 9
- E. Siku 10 hadi 19
- F. Siku 20 hadi 29
- G. Siku zote 30

53. Katika siku 30 zilizopita, kwa siku ulizokunywa pombe, mara ngapi **kwa kawaida** ulikunywa kwa siku?

- A. Sikunywa pombe katika siku 30 zilizopita
- B. Pungufu ya mara 1
- C. Mara 1
- D. Mara 2**
- E. Mara 3
- F. Mara 4
- G. Mara 5 au zaidi

54. Katika siku hizo 30 zilizopita, ulipataje **kwa kawaida** pombe hiyo uliyokunywa? CHAGUA JAWABU MOJA TU.

- A. Sikunywa pombe katika hizo siku 30 zilizopita
- B. Niliinunua katika kibanda, duka, au kutoka kwa muuzaji wa barabarani
- C. Nilimpa mtu mwingine fedha kuninunulia
- D. Nilipewa na marafiki zangu
- E. Nilipewa nyumbani
- F. Niliiba
- G. Nilitengeneza mwenyewe
- H. Nilipata kwa njia nyingine

55. Nani **kwa kawaida** unayekunywa naye pombe?

- A. Sinywi pombe
- B. Marafiki zangu
- C. Familia yangu
- D. Watu ninaokutana nao tu
- E. Kwa kawaida nakunywa peke yangu

56. Ni aina gani ya pombe kwa kawaida unayokunywa? CHAGUA JAWABU MOJA TU.

- A. Sinywi pombe
- B. Bia, Safari larger, au Stout
- C. Mvinyo
- D. Pombe kali kama vile konyagi
- E. Pombe iliyotengenezwa kienyeji
- F. Pombe kali zilizotengenezwa kienyeji
- G. Aina nyingine

57. Katika maisha yako, mara ngapi ulikunywa pombe sana hadi ukalewa chakari?

- A. Mara 0
- B. Mara 1 au 2
- C. Mara 3 hadi 9
- D. Mara 10 au zaidi

58. Katika maisha yako, mara ngapi umewahi kubaki na uchovu, kujisikia kuumwa, kugombana na familia yako au marafiki, kukosa shule, au kupigana, kama matokeo ya kunywa pombe?

- A. Mara 0
- B. Mara 1 au 2
- C. Mara 3 hadi 9
- D. Mara 10 au zaidi

59. Nani kati ya wazazi au walezi wako wanakunywa pombe?

- A. Hakuna
- B. Baba au mlezi wa kiume
- C. Mama au mlezi wa kike
- D. Wote
- E. Sijui

60. Kuna yeyote katika familia yako aliyejadiliana nawe kuhusu madhara ya kunywa pombe?

- A. Ndiyo
- B. Hapana

61. Katika mwaka huu wa masomo, ulifundishwa katika somo lolote kuhusu hatari za kutumia pombe?

- A. Ndiyo
- B. Hapana
- C. Sijui

Maswali mawili yafuatayo yanahusu dawa za kulevya.

62. Katika maisha yako, mara ngapi umetumia dawa za kulevya, kama bangi au kokeni?

- A. Mara 0
- B. Mara 1 au 2
- C. Mara 3 hadi 9
- D. Mara 10 au zaidi

63. Katika mwaka huu wa masomo, ulifundishwa katika somo lolote kuhusu athari za kutumia dawa za kulevya kama bangi au kokeni?

- A. Ndiyo
- B. Hapana
- C. Sijui

Maswali 12 yafuatayo yanahusu kujamiiana na virusi vya UKIMWI au UKIMWI.

64. Umewahi kujamiiana?

- A. Ndiyo
- B. Hapana

65. Ulikuwa na umri gani ulipojamiiana kwa mara ya kwanza?

- A. Sijawahi kujamiiana
- B. Miaka 11 au pungufu
- C. Miaka 12
- D. Miaka 13
- E. Miaka 14
- F. Miaka 15
- G. Miaka 16 au zaidi

66. Katika maisha yako, umejamiiana na watu wangapi?

- A. Sijawahi kujamiiana
- B. Mtu 1
- C. Watu 2
- D. Watu 3
- E. Watu 4
- F. Watu 5
- G. Watu 6 au zaidi

67. Katika miezi 12 iliyopita, umewahi kujamiiana?

- A. Ndiyo
- B. Hapana

68. Kwa **mara ya mwisho** ulipojamiiana, wewe au mwenzi wako alitumia kondomu?

- A. Sijawahi kujamiiana
- B. Ndiyo
- C. Hapana

69. **Kama** wewe ungetaka kupata kondomu, ungeipataje hasa?

- A. Ningeipata kutoka kwenye mashine ya kuuzia
- B. Ningeipata katika kibanda au duka au kutoka kwa muuzaji wa barabarani
- C. Ningeipata kutoka duka la dawa, kliniki au hospitali
- D. Ningempa mtu mwingine fedha kuninunulia
- E. Ningeipata kwa njia nyingine
- F. Sijui

70. **Kama** wewe ungetaka kupata dawa/njia ya kuzuia mimba, ungeipataje hasa?

- A. Ningeipata kutoka kwenye mashine ya kuuzia
- B. Ningeipata katika kibanda au duka au kutoka kwa muuzaji wa barabarani
- C. Ningeipata kutoka duka la dawa, kliniki au hospitali
- D. Ningempa mtu mwingine fedha kuninunulia
- E. Ningeazima kutoka kwa mtu mwingine
- F. Ningeipata kwa njia nyingine
- G. Sijui

71. Umewahi kusikia kuhusu Virusi vya UKIMWI au ugonjwa wa UKIMWI?

- A. Ndiyo
- B. Hapana

72. Je, watu wanaweza hupata Virusi vya UKIMWI au UKIMWI kwa kutokana na kuumwa na mbu?

- A. Ndiyo
- B. Hapana
- C. Sijui

73. Je, mtu anayeonekana mwenye afya anaweza kuwa na Virusi vya UKIMWI?

- A. Ndiyo
- B. Hapana
- C. Sijui

74. Katika mwaka huu wa masomo, ulifundishwa katika somo lolote jinsi ya kuepukana na Virusi vya UKIMWI au UKIMWI?

- A. Ndiyo
- B. Hapana
- C. Sijui

75. Umewahi kuongea kuhusu maambukizo ya Virusi vya UKIMWI au UKIMWI na wazazi au walezi wako?

- A. Ndiyo
- B. Hapana

Maswali 3 yafuatayo yanahusu mazoezi ya viungo. Mazoezi ya viungo ni mazoezi yoyote ambayo huongeza mapigo ya moyo na mara nyingine hukufanya kuhema. Mazoezi ya viungo yanaweza kufanywa kwa michezo, kucheza na marafiki, au kutembea kwenda shuleni. Baadhi ya mifano ya mazoezi ya viungo ni kukimbia, kutembea haraka, kuendesha baiskeli, kucheza dansi, mpira wa miguu, mpira wa mikono, kuruka kamba, na kuogelea.

JUMLISHA MUDA WOTE UNAOTUMIA KATIKA MAZOEZI YA VIUNGO KWA SIKU. **USIHESABIE** SOMO LA MICHEZO.

76. Katika **siku 7** zilizopita, kwa siku ngapi ulifanya mazoezi ya viungo kwa jumla ya angalau dakika 60 kwa siku?

- A. Siku 0
- B. Siku 1
- C. Siku 2
- D. Siku 3
- E. Siku 4
- F. Siku 5
- G. Siku 6
- H. Siku 7

77. Katika wiki ya **kawaida**, kwa siku ngapi unafanya mazoezi ya viungo kwa jumla ya angalau dakika 60 kwa siku?

- A. Siku 0
- B. Siku 1
- C. Siku 2
- D. Siku 3
- E. Siku 4
- F. Siku 5
- G. Siku 6
- H. Siku 7

78. Katika mwaka huu wa masomo, ulifundishwa katika somo lolote kuhusu faida za mazoezi ya viungo?

- A. Ndiyo
- B. Hapana
- C. Sijui

Swali lifuatalo linahusu muda unaotumia kwa kukaa tu wakati haupo shuleni au hufanyi kazi za nyumbani.

79. Muda gani unatumia katika siku ya **kawaida** kwa kukaa na kuangalia luninga, kucheza michezo ya kompyuta, kuongea na marafiki, au kufanya shughuli nyingine za kukaa, kama vile kucheza karata, kusuka nywele, au kufuma?

- A. Pungufu ya saa 1 kwa siku
- B. Saa 1 hadi 2 kwa siku
- C. Masaa 3 hadi 4 kwa siku
- D. Masaa 5 hadi 6 kwa siku
- E. Masaa 7 hadi 8 kwa siku
- F. Masaa 8 au zaidi kwa siku

Maswali 2 yafuatayo yanahusu kwenda na kurudi nyumbani kutoka shuleni.

80. Katika siku 7 zilizopita, kwa siku ngapi ulitembea au kuendesha baiskeli kwenda na kurudi kutoka shuleni?

- A. Siku 0
- B. Siku 1
- C. Siku 2
- D. Siku 3
- E. Siku 4
- F. Siku 5
- G. Siku 6
- H. Siku 7

81. Katika siku 7 zilizopita, muda gani **kwa kawaida** ulichukua kwa kwenda na kurudi kutoka shuleni kila siku? JUMLISHA MUDA ULIOTUMIA KWENDA NA KURUDI NYUMBANI KUTOKA SHULENI.

- A. Pungufu ya dakika 10 kwa siku
- B. Dakika 10 hadi 19 kwa siku
- C. Dakika 20 hadi 29 kwa siku
- D. Dakika 30 hadi 39 kwa siku
- E. Dakika 40 hadi 49 kwa siku
- F. Dakika 50 hadi 59 kwa siku
- G. Dakika 60 au zaidi kwa siku

Maswali 5 yafuatayo yanahusu uzoefu wako shuleni na nyumbani.

82. Katika siku 30 zilizopita, kwa siku ngapi ulikosa masomo au shule bila ruhusa?

- A. Siku 0
- B. Siku 1 au 2
- C. Siku 3 hadi 5
- D. Siku 6 hadi 9
- E. Siku 10 au zaidi

83. Katika siku 30 zilizopita, mara ngapi wanafunzi wengi katika shule walionyesha wema na kutoa msaada?

- A. Hakuna
- B. Mara chache sana
- C. Mara chache
- D. Mara nyingi sana
- E. Daima

84. Katika siku 30 zilizopita, mara ngapi wazazi au walezi wako walifuatilia kuona kama umefanya kazi zako za nyumbani?

- A. Hakuna
- B. Mara chache sana
- C. Mara chache
- D. Mara nyingi sana
- E. Daima

85. Katika siku 30 zilizopita, mara ngapi wazazi au walezi wako waliyaelewa matatizo na masikitiko yako?

- A. Hakuna
- B. Mara chache sana
- C. Mara chache
- D. Mara nyingi sana
- E. Daima

86. Katika siku 30 zilizopita, mara ngapi wazazi au walezi wako walifahamu **haswa** nini ulichokuwa unafanya wakati wako wa mapumziko?

- A. Hakuna
- B. Mara chache sana
- C. Mara chache
- D. Mara nyingi sana
- E. Daima